

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA LUDEWA



LUDEWA

Oktoba 25, 2022

TAARIFA KWA UMMA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Ndg. Sunday Deogratias akiambatana na Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Ludewa Bwn. Linus Malamba akimuwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Ludewa Mhe. Andrea Tsere wamempokea Mkuu Mkoa wa Njombe Mhe. Anthony Mtaka ambaye amekuwa na ziara ya kikazi ya siku mbili ndani ya Wilaya ya Ludewa.

Jana Oktoba 24, 2022 Mkuu wa Mkoa wa Njombe aliambatana na wataalamu mbalimbali wakiongozwa na Mkurugenzi wa Viwanda mama kutoka Shirika la Maendeleo ya Taifa (NDC) Bwn. Yohana Mtoni waliokuja kwaajili ya kuzungumza na wananchi wa Tarafa ya Liganga wanaozungukwa na Madini ya Chuma katika Kata ya Mundindi na Wananchi wa Tarafa ya Masasi waliozungukwa na Madini ya Makaa ya Mawe katika Kata ya Nkomang'ombe.

Lengo la ziara hiyo ni kuanza kwa uhakiki wa ulipwaji wa fidia kwa wananchi wanaozungukwa na mradi wa Liganga ambapo kuna madini ya chuma na mchuchuma na kwenye Mradi wa Makaa ya Mawe.

Wakati akizungumza na wananchi wa maeneo hayo Mkuu wa Mkoa wa Njombe Mhe. Anthony Mtaka amewataka wananchi kujipanga kufanya maendeleo yenye tija kwao wenyewe, kwa Wilaya , Mkoa wa Njombe na Taifa kwa Ujumla.

A handwritten signature in blue ink.

Chrispin B. Kalinga
Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini
Wilaya ya Ludewa.